NISHATI | HABARI ZA NISHATI
News Bulletin
www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati
Toleo Namba 35 Februari 1 - 28, 2022

# TPDC, Baker Botts waingia mkataba majadiliano LNG




*Waziri wa Nishati, January Makamba (wa kwanza kushoto waliosimama) na Mwenyekiti wa Majadiliano ya mradi wa LNG kwa upande wa Serikali ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mhandisi Charles Sangweni (wa pili kulia waliosimama) wakishuhudia Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya Baker Botts (UK) LLP wakisaini Mkataba wa Huduma ya Ushauri wa Kitaalam ili kushirikiana katika majadiliano ya kutekeleza Mradi wa LNG unaotarajiwa kutekelezwa eneo la Likong'o mkoani Lindi. Wanaotia saini ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt.James Mataragio na Hamish McArdle kutoka kampuni ya Baker Botts LLP.*

LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma



# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Mhandisi Felchesmi Mramba**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**

Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma





*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# TPDC, Baker Botts waingia mkataba majadiliano LNG




*Waziri wa Nishati, January Makamba (wa kwanza kushoto waliosimama) na Mwenyekiti wa Majadiliano ya mradi wa LNG kwa upande wa Serikali ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mhandisi Charles Sangweni (wa pili kulia waliosimama) wakishuhudia Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya Baker Botts (UK) LLP wakisaini Mkataba wa Huduma ya Ushauri wa Kitaalam ili kushirikiana katika majadiliano ya kutekeleza Mradi wa LNG unaotarajiwa kutekelezwa eneo la Likong'o mkoani Lindi. Wanaotia saini ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt.James Mataragio na Hamish McArdle kutoka kampuni ya Baker Botts LLP.*

**Na Janeth Mesomapya**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya Baker Botts (UK) LLP wamesaini Mkataba wa Huduma ya Ushauri wa Kitaalam na Kampuni ya Baker Botts (UK) LLP ya Uingereza ili kushirikiana na Serikali katika majadiliano ya kutekeleza Mradi wa kubadili Gesi asilia kuwa katika hali ya kimiminika (LNG).

Hafla ya utiaji saini wa mkataba huo ilifanyika Januari 25, 2022 jijini Arusha huku ikishuhudiwa na Waziri wa Nishati January Makamba, Mwenyekiti wa Majadiliano kwa upande wa Serikali ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mhandisi Charles Sangweni, viongozi wa Serikali, na wadau mbalimbali wa sekta ya nishati nchini.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini wa makubaliano hayo, Waziri Makamba alisema kuwa kampuni hiyo ya Baker Botts ni kampuni kubwa ya kisheria na kitaalamu ambayo imebobea katika kutoa ushauri wa masuala ya mafuta na gesi kwenye nchi mabalimbali duniani.

"Baada ya kusaini mkataba huu, imani yetu ni kwamba mazungumzo haya yataenda haraka na kwa ufanisi zaidi na Serikali itapata mkataba ambao

**"Mradi huu pia utasaidia kuiingiza Tanzania katika ramani ya dunia ya nchi zenye nguvu ya ushawishi kutokana na kuwa na nishati ambayo inatumika na inahitajika duniani."**

# TPDC, Baker Botts waingia mkataba majadiliano LNG

utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi yetu," alieleza Waziri Makamba

Aidha, alieleza kuwa majadiliano kuhusu uwekezaji wa LNG baina ya Serikali na washirika wa mradi huo yanaendelea vizuri na kwamba kuna matumaini makubwa kuwa mradi huo utafanikiwa huku pande zote mbili zikikubaliana kuhusu haja ya kuharakisha mazungumzo hayo huku wakizingatia ufanisi, weledi na uangalifu mkubwa.

Waziri Makamba aliongeza kuwa majadiliano hayo yanahusu manufaa yatakayotokana na mradi huo wa LNG ikiwa ni pamoja na kipato kwa serikali, uwezo wa Watanzania kuijua sekta pamoja na ushirikishwaji wa wazawa katika kutoa huduma na bidhaa katika kipindi kizima cha utekelezwaji wa mradi.

"Mradi huu pia utasaidia kuiingiza Tanzania katika ramani ya dunia ya nchi zenye nguvu ya ushawishi kutokana na kuwa na nishati ambayo inatumika na inahitajika duniani," aliongeza.

Alibainisha pia kuwa manufaa mengine ni pamoja na gesi itakayozalishwa kutumika katika kumaliza changamoto ya uzalishaji wa umeme nchini kutokana na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha gesi asilia.

Kwa upande wake Mha. Sangweni alieleza kuwa majadiliano hayo yamejikita katika maeneo makuu manne ambayo ni ya kisheria, kiufundi, kiuchumi pamoja na eneo la masoko.

"Serikali imedhamiria kutekeleza mradi huu na tumepewa muda wa mwaka mmoja kuhakikisha tumefikia muafaka wa majadiliano haya baina ya serikali na wawekezaji wa mradi huu," aliongeza.

Mradi wa LNG unakadiriwa kuwa wa thamani ya takriban Dola za Marekani bilioni 30 huku wabia wake wakuu wakiwa ni kampuni za Equinor, Shell na TPDC kwa niaba ya serikali ambao ni waendeshaji wa vitalu namba 1, 2 na 4.



*Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio (kulia) na Hamish McArdle (kushoto) kutoka kampuni ya Baker Botts LLP wakipeana mkono wa pongezi mara baada ya kusaini mkataba wa huduma ya ushauri wa kitaalam katika majadiliano ya mradi wa kubadili Gesi asilia kuwa katika hali ya kimiminika (LNG) unaotarajiwa kutekelezwa eneo la Likong'o mkoani Lindi. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Nishati, January Makamba (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Majadiliano ya mradi wa LNG kwa upande wa Serikali ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mhandisi Charles Sangweni (wa pili kulia).*

# MAKAMBA AKUTANA NA MENEJIMENTI YA WIZARA



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto) akimpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kulia) mara baada ya kuwasili Makao Makuu ya Wizara ya Nishati jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022, katikati Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*

**Hafsa Omar- Dodoma**

Waziri wa Nishati, January Makamba amekutana na menejimenti ya Wizara ya Nishati, mara baada ya mapokezi ya Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

Kikao kilifanyika tarehe 10 Januari, 2022 katika ofisi za Wizara zilizopo Mtumba jijini Dodoma.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara hiyo na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

Akizungumza katika kikao hicho, Makamba





*Waziri wa Nishati, January Makamba akiongoza kikao cha Menejimenti ya Wizara ya Nishati kilichofanyika Makao Makuu ya Wizara ya Nishati jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*

# MAKAMBA AKUTANA NA MENEJIMENTI YA WIZARA

alimpongeza Katibu Mkuu wa Wizara kwa uteuzi wake alioupata hivi karibuni na kumtaka kufanya kazi kwa weledi na uadilifu.

Pia, aliwataka viongozi wa Wizara pamoja na wa Taasisi kusimamia miradi yote ya Nishati ili ikamilike kwa wakati na watanzania wafaidike na miradi hiyo.

Vilevile, aliwataka watumishi wa Wizara na Taasisi zake kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kuleta matokeo chanya yenye tija ambayo yataleta mabadiliko nchini.

Naye, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alitoa pongezi zake kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo na kumtakia majukumu mema.



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto) akiwa katika mazungumzo na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (katikati) Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kulia) pamoja na Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (hayupo pichani) kabla ya kuanza kikao cha Menejimenti ya Wizara kilichofanyika Makao Makuu ya Wizara ya Nishati Jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba aliwashukuru Watumishi wote wa Wizara hiyo kwa mapokezi waliyomuandalia wakati alipowasili wizarani.

Aidha, aliahidi kutoa ushirikiano kwa watumishi wa Wizara hiyo na kuwataka kumuunga mkono katika majukumu yake.



*Waziri wa Nishati, January Makamba, akizungumza katika kikao cha Menejimenti cha Wizara ya Nishati kilichofanyika Makao Makuu ya Wizara ya Nishati Jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, akizungumza katika kikao cha Menejimenti ya Wizara ya Nishati kilichofanyika Makao Makuu ya Wizara ya Nishati Jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*

# Naibu Waziri akerwa na kasi ndogo ujenzi wa kituo cha umeme

**Na Timotheo Mathayo, Morogoro**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ametembelea ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme pamoja na laini mpya za kusambaza umeme kinachojengwa wilaya ya Ifakara mkoani Morogoro.

Ziara hiyo ilifanyika tarehe ilifanyika 26 Januari 2022 ambapo alikagua mradi huo unaojengwa na mkandarasi AEE POWER EPC kutoka nchini Hispania.

Mkandarasi huyo alijenga kituo cha kupoza umeme wakati ambapo njia za kusambaza umeme zinajengwa na mkandarasi Burhani kutoka nchini Kenya kwa ufadhili wa Umoja wa nchi za Ulaya (EU) pamoja na fedha kutoka Serikali kuu ambapo jumla ya shilingi Bilioni 14 zitatumika.

Meneja wa TANESCO, Wilaya ya Kilombero, Hamza Almas alisema ujenzi wa kituo cha kupoza umeme kitakuwa na mashineumba moja yenye ukubwa wa 220/33kv, 20MVA na kitatoa laini kubwa za msongo wa kilovoti 33, laini moja itatoa huduma wilaya ya Ulanga na nyingine tatu zitatumika Ifakara katika wilaya ya Kilombero.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa Tatu kulia) akikagua kazi za ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme pamoja na laini mpya za kusambaza umeme kinachojengwa wilaya ya Ifakara mkoani Morogoro.*

Katika ziara hiyo, Naibu waziri hakuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi huo na alitoa maelekezo kwa mkandarasi mjenzi wa mradi huo kuwepo eneo la mradi muda wote ili akamilishe kazi kwa wakati kwa kuwa serikali inamlipa kwa wakati.

Alisema TANESCO itazame taratibu zote za kimkataba ili mkandarasí huyo akishidwa kutekeleza mradi kwa wakati akatwe asilimia Kumi ya gharama za ujenzi wa mradi kama ilivyoainishwa katika mkataba.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigodi alisema mara kwa mara amekuwa akifuatilia ujenzi wa mradi huo lakini mkandarasi mara nyingi amekuwa haonekani kwenye eneo la mradi, jambo linalotia hofu kama ataweza kukamilisha ujenzi kwa wakati.

Aidha Naibu Waziri alifanya ziara ya kukagua bwawa la kuzalisha umeme la Kidatu kuona wingi wa maji na kama kiasi cha maji yaliyomo yataweza kukidhi mahitaji ya umeme yanayohitajika.

Byabato aliridhishwa na kiwango cha maji yaliyomo katika bwawa hilo na wataalam kutoka TANESCO walisema ujazo uliopo katika bwawa la Kidatu kwa sasa unatosha kuzalisha umeme.

# KATIBU MKUU NISHATI AFUNGUA RASMI KIKAO KAZI NGAZI YA MAKATIBU WAKUU

**Hafsa Omar- Dodoma**

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amefungua rasmi kikao kazi ngazi ya Makatibu Wakuu na wakuu wa Taasisi wadau, kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu.

Kikao hicho kilifanyika tarehe 25 Januari, 2022 katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma.



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati) akiendesha kikao kazi ngazi ya Makatibu Wakuu na wakuu wa Taasisi kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu, kilichofanyika tarehe 25 Januari, 2022 katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma.*

Makatibu Wakuu ambao wapo katika timu hiyo ni kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na



*Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kulia) akizungumza katika kikao kazi ngazi ya Makatibu Wakuu na wakuu wa Taasisi kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu kilichofanyika tarehe 25 Januari, 2022 katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma. Kushoto wa kwanza Naibu katibu Mkuu ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Abdallah Mitawi.*



*Wajumbe kutoka Taasisi mbalimbali wakiwa katika kikao kazi ngazi ya Makatibu Wakuu na wakuu wa Taasisi kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu kilichofanyika tarehe 25 Januari, 2022 katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma.*

# KATIBU MKUU NISHATI AFUNGUA RASMI KIKAO KAZI NGAZI YA MAKATIBU WAKUU

**"Makatibu Wakuu ambao wapo katika timu hiyo ni kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba Maendeleo ya Makazi, na Na wakuu taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo."**



*Baadhi ya washiriki wa kikao kazi ngazi ya Makatibu Wakuu na wakuu wa Taasisi kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu kilichofanyika tarehe 25 Januari, 2022 katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma.*

Na wakuu taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo.

Akizungumza katika kikao hicho Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Mramba alisema, Ikolojia ya Mabonde ya Rufiji na Pangani ni muhimu kwa ustawi wa Taifa kutokana na umuhimu wake katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta za nishati, maji, maliasili na utalii, mazingira, kilimo, mifugo, na uvuvi.

Aliongeza kuwa, Mabonde hayo ni muhimu kwa uzalishaji wa nishati ya umeme wa maji ambapo asilimia 36 ya umeme unaozalishwa nchini megawati 573 inatokana na chanzo cha maji katika Mabonde hayo.

Alieleza kuwa, gharama za uzalishaji wa umeme kutokana na vyanzo vya maji ni wastani wa shilingi 13 kwa uniti ikilinganishwa na gharama za uzalishaji wa umeme kwa kutumia Gesi asilia ambazo ni kati ya shilingi 129 na 153 kwa uniti na kwa kutumia mafuta ya dizeli ni kati ya shilingi 546 na 675 kwa uniti.

Aidha, alisema ili kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu, Serikali imeendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji wa umeme kupitia vyanzo vya maji vilivyopo nchini.

Katika jitihada hizo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere megawati 2,115 ambapo baada ya kukamilika kwa mradi huu, uzalishaji wa umeme kwa vyanzo vya maji utakuwa ukichangia zaidi ya asilimia 73 ya umeme wote utakaokuwa ukizalishwa nchini.

Alifafanua kuwa, pamoja na umuhimu wa vyanzo vya maji katika uzalishaji wa nishati ya umeme, vyanzo hivyo vimekuwa vikikabiliwa na changamoto mbalimbali kutokana na uwepo wa shughuli za kibinadamu zisizoendelevu katika mabonde hayo pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alieleza kuwa, kwa kutambua umuhimu wa kuhifadhi mabonde hayo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, tarehe 13 Aprili, 2017, wakati huo akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# KATIBU MKUU NISHATI AFUNGUA RASMI KIKAO KAZI NGAZI YA MAKATIBU WAKUU

aliagiza hatua za haraka zichukuliwe kwa lengo la kuokoa Ikolojia ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu ili kuokoa mfumo wa Ikolojia wa Bonde la Mto huo.

Pia,alisema Wizara ya Nishati inatambua jitihada zilizochukuliwa na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi kuhakikisha suala la utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa vyanzo vya maji katika Mabonde ya Pangani na Rufiji unazingatiwa.

Vile vile, alisisitiza kuwa kwa kutambua jitihada zilizofanywa na Serikali na kwa kuzingatia maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa kuhusu utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa vyanzo vya maji nchini pamoja na uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa mabwawa ya kuzalisha umeme uliofanywa na Serikali hususani katika Mabonde ya Pangani na Rufiji.

Wizara ya Nishati iliandaa kikao kazi kwa ngazi ya wataalamu kuhusu uimarishaji wa usimamizi wa rasilimali maji katika Mabonde ya hayo, kikao hicho kilifanyika tarehe 16 hadi 21 mwaka jana, ambapo wataalamu hao walifanya kazi na kutoa mapendekezo mbalimbali ya usimamizi na matumizi ya rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu.





*Picha mbalimbali za matukio katika katika kikao kazi ngazi ya Makatibu Wakuu na wakuu wa Taasisi kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali maji katika mabonde ya Rufiji na Pangani ili kuwezesha upatikanaji wa Nishati endelevu kilichofanyika tarehe 25 Januari, 2022 katika Ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma.*

# AfDB yatembelea Mradi wa umeme wa Zuzu, yaipongeza Wizara ya Nishati

**Na Zuena Msuya, Dodoma**

Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika nchini Tanzania, Amos Cheptoo ameipongeza Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kusimamia ipasavyo fedha zilizotolewa na benki hiyo kutekeleza miradi ya umeme inayoendelea nchini.

Cheptoo alitoa pongezi hizo Januari 25, 2022 wakati alipofanya ziara katika Kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu kilichopo mkoani Dodoma. Katika ziara hiyo, aliambatana na ujumbe wake pamoja na Maafisa waandamizi kutoka Wizara ya Nishati na TANESCO.

Cheptoo alisema kuwa, lengo la ziara hiyo ni kukagua miradi ya umeme inayofadhiliwa na Benki hiyo ili kuona utekelezaji wake na hatua iliyofikiwa kutokana na fedha zinazotolewa na Benki hiyo.

Baada ya kuona hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo, alieleza kuwa miradi hiyo imefikia hatua nzuri za utekelezaji wake, pia AfDB imeahidi kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ya Ujenzi, Maji na Nishati.

Awali kabla ya kutembelea miradi hiyo, Mkurugenzi huyo wa AfDB alipata wasaa wa kujitambulisha na kuzungumza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba ambapo pamoja na mambo mengine alimhakikishia Katibu Mkuu huyo kuwa, Benki hiyo ipo tayari kuendelea kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo ya aina hiyo kwa lengo la kuiwezesha



*Mkurugenzi wa Benki ya Afrika ya Maendeleo (AfDB), nchini Tanzania, Amos Cheptoo (wa pili kushoto) akipata maelezo ya utekelezaji wa mradi wa umeme wa Zuzu, kutoka kwa Mhandisi Mkaazi wa Mradi huo kutoka Kampuni ya GOPA, Mhandisi Clive Sihwa, wakati wa ziara ya kutembelea mradi huo, mkoani Dodoma, Januari 25,2022.*



*Mkurugenzi wa Benki ya Afrika ya Maendeleo (AfDB), nchini Tanzania, Amos Cheptoo (katikati) akizungumza na ujumbe wake pamoja na Maafisa waandamizi kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakati wa ziara ya kutembelea Mradi wa umeme wa Zuzu mkoani Dodoma, Januari 25,2022.*

# AfDB yatembelea Mradi wa umeme wa Zuzu, yaipongeza Wizara ya Nishati

Tanzania kutimiza azma yake ya kuwapatia wananchi wake nishati ya umeme ya kutosha, na ya bei nafuu.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Mramba aliishukuru Benki hiyo kwa ushirikiano na mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza sekta ya nishati nchini,na kwamba wataendelea kuitumia Benki hiyo katika ufadhili wa miradi mbalimbali ya nishati inayohitaji fedha katika utekelezaji wake.

Alisema kuwa, Tanzania kama nchi inayoendelea kukua inahitaji zaidi nishati ya umeme katika kuhakikisha kuwa uchumi wake unakua kwa kuwa na umeme wa uhakika, kutosha na wa gharama nafuu ili kutimiza malengo iliyojiwekea.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Benki ya Afrika ya Maendeleo (AfDB) nchini Tanzania, Amos Cheptoo (kushoto kwa Katibu Mkuu), pamoja na viongozi waandamizi wa Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na ujumbe ulioambatana na mkurugenzi huyo wa AfDB, walipofika kujitambulisha kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Januari 25,2022.*



*Mkurugenzi wa Benki ya Afrika ya Maendeleo (AfDB), nchini Tanzania, Amos Cheptoo (wa tatu kushoto) akikagua mradi wa umeme wa Zuzu wakati wa ziara ya kutembelea mradi huo, mkoani Dodoma, Januari 25,2022.*

Hata hivyo aliendelea kusema kuwa AfDB, imetoa mchango mkubwa katika miradi ya kuzalisha, kusambaza na kusafirisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

Alitaja baadhi ya miradi inayofadhiliwa na AfDB, itakayozalisha umeme kwa kutumia maji pindi itakapokamilika kuwa ni pamoja na Mradi wa Kakonko na Malagarasi.

Aidha mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa msongo wa Kilovolti 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga, na Tanzania hadi Kenya aliitaja kuwa ni mojawapo ya miradi iliyofadhiliwa na Benki ya AfDB pamoja na mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovolti 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi, na Nyakanazi hadi Kigoma wenye msongo wa Kilovolti 400.

Katibu Mkuu Mramba, alisema kuwa licha ya AfDB kufadhili miradi hiyo moja kwa moja, pia kuna baadhi ya miradi mingine imeifadhili kwa kushirikiana na washirika wengine wa maendeleo ikiwemo Shirika la Maendeleo la Japani (JICA).

# WAZIRI MAKAMBA ATOA WITO INDIA KUWEKEZA SEKTA YA NISHATI

**Na Janeth Mesomapya**

Waziri wa Nishati, January Makamba ametoa wito kwa serikali ya India na wawekezaji wa nchini humo kutembelea nchini Tanzania ili kutazama fursa zinazopatikana kwenye maeneo mbalimbali ya sekta ya nishati ikiwa ni pamoja na zile za kitalu cha Mnazi Bay North ili kufanya uwekezaji.

Waziri Makamba aliyasema hayo, Januari 5, 2022 alipokutana na Balozi wa India nchini Tanzania Mhe. Binaya Pradhan katika ofisi za Wizara jijini Dar es Salaam. Mazungumzo yao yalilenga kujadili ushirikiano kwa kisekta baina ya Tanzania na India.

Alieleza kuwa, zipo fursa za uwekezaji kwenye kitalu hicho ambazo zinahitaji uwekezaji wa haraka na hivyo wafanyabiashara na wawekezaji hao wajitokeze ili kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) katika



*Waziri wa Nishati, January  Makamba (kulia) akifanya mazungumzo na Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan (katikati) baada ya kukutana Januari 5, 2022 katika ofisi za Wizara jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Katibu wa Balozi Raj Ganger.*



*Waziri wa Nishati, January Makamba (kushoto) akimsikiliza Balozi wa India nchini Tanzania Mhe. Binaya Pradhan wakati wa mazungumzo yao yaliyofanyika Jumatano, Januari 5, 2022 katika ofisi za Wizara jijini Dar es Salaam. Pamoja nao ni Katibu wa Balozi Raj Ganger (Kulia). Wengine (kutoka kulia) ni Meneja Huduma za Sheria wa REA, Mussa Muze, Naibu Mkurugenzi wa Uzalishaji Umeme wa TANESCO, Pakaya Mtamakaya, Afisa Mazingira wa TANESCO Agripina Focus na Katibu wa Waziri wa Nishati, Wakili Dunford Mpelumbe.*

# WAZIRI MAKAMBA ATOA WITO INDIA KUWEKEZA SEKTA YA NISHATI

kuzitumia fursa husika.

Vivyohivyo, alisema zipo fursa za uwekezaji kwenye miradi ya nishati ya jua na ujenzi wa maghala ya kutunzia mafuta ambayo ni hitaji kubwa kwa Tanzania na inaweza kutumika kimkakati kusambaza mafuta katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

"Nawakaribisha sana wawekezaji wa India kuwekeza katika fursa za maghala ya mafuta kwa kushirikiana na kampuni ya kuhifadhi mafuta (Tiper) kwa kutumia miundombinu yake ambayo tayari imeshajengwa, kikubwa ikiwa ni kuzingatia uboreshaji wa miundombinu hiyo," alifafanua Waziri Makamba.

Kwa upande wake, Balozi Pradhan alisema Serikali ya India itaendelea kushirikiana na Tanzania ikiwa ni pamoja na kuwahimiza wafanyabiashara na wawekezaji wake kuchangamkia fursa mbalimbali zinazopatikana nchini.

Alieleza kuwa, kwa sasa Serikali hiyo inatazamia kuwekeza nchini Tanzania kwenye eneo la maghala ya mazao ya petroli, fursa zinazotokana na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda hadi Chongoleani Tanzania (EACOP) pamoja na miradi ya umeme wa jua (Solar) ukiwemo ule wa wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

"Serikali ya India kwa kushirikiana na sekta binafsi imejipanga kuendelea kufanya uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali ya kimaendeleo duniani kote, ikiwemo nchini Tanzania," aliongeza.




*Waziri wa Nishati, January Yusuph Makamba (kulia) akiwa na Balozi wa India nchini Tanzania Mhe. Binaya S. Pradhan baada ya kukutana na kufanya mazungumzo Januari 5, 2022 katika ofisi za Wizara jijini Dar es Salaam.*

# KATIBU MKUU NISHATI APOKELEWA RASMI WIZARANI

Uongozi wa Wizara ya Nishati pamoja na watumishi wa Wizara wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mbahimbali wamempokea Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba ambaye ameapishwa rasmi kuwa katibu Mkuu wa Wizara.

Mhandisi Mramba aliapishwa rasmi na Rais ya Jamhuri wa Muungano Samia Suluhu Hassan tarehe 10 Januari 2022 jijini Dodoma.

## Picha za matukio mbalimbali wakati wa kupolewa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kulia) akipokea shada la maua mara baada ya kuwasili Makao Makuu ya Wizara ya Nishati jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (kulia) akisalimiana na Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali mara baada ya kuwasili Makao Makuu ya Wizara ya Nishati jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na watumishi mbalimbali wa Wizara ya Nishati mara baada ya kuwasili Makao Makuu ya Wizara ya Nishati jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*



*Katibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi (katikati waliokaa) Mramba akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati pamoja na watumishi wa Wizara, mara baada ya kuwasili Makao Makuu ya Wizara ya Nishati jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*

# Picha za matukio mbalimbali wakati wa kupolewa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati









*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akisalimiana na watumishi mbalimbali mara baada ya kuwasili Makao Makuu ya Wizara ya Nishati jijini Dodoma tarehe 10 Januari 2022.*

# MAKABIDHIANO YA OFISI YA KATIBU MKUU

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja amekabidhi ofisi kwa Katibu Mkuu Mpya wa Wizara, Mhandisi Felchesmi Mramba.

Mhandisi Felchesmi Mramba aliteuliwa kushika nafasi ya Ukatibu Mkuu wa Wizara hiyo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suhuhu Hassani Januari 8, 2022 na kuapishwa Januari 10, 2022 katika viwanja vya Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma.

Makabidhiano hayo yalifanyika katika ofisi za Wizara hiyo katika Mji wa Serikali Mtumba, Januari 11, 2022.

Makabidhiano hayo yalishuhudiwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara hiyo, Kheri Mahimbali na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu, Ziana Mlawa.

Katika makabidhiano hayo, Masanja aliwashukuru watumishi wote wa Wizara hiyo kwa ushirikiano waliomuonyesha wakati wa Uongozi wake.

Hata hivyo alimhakikishia Katibu Mkuu Mpya ushirikiano pale atakapokuwa akiuhitaji kwa maslahi ya Taifa katika Sekta ya Nishati.

Vilevile alitoa wito kwa watumishi wa Wizara hiyo kutoa ushirikiano kwa kiongozi huyo mpya pamoja na kufanya kazi kwa kuzingatia weledi juhudi na kwa kasi zaidi.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa pili kushoto) na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Leonard Masanja (wa pili kulia) wakifanya makabidhiano ya ofisi. Wengine katika picha ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Kheri Mahimbali (kushoto) na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu, Ziana Mlawa.*

# Jamii yatakiwa kutunza mazingira kuzunguka mabwawa ya umeme

**Na Timotheo Mathayo, Iringa.**

Jamii inayozunguka mradi wa bwawa la kufua umeme la Kihansi lililopo mkoani Iringa wametakiwa kulinda na kutunza mazingira ili mradi huo uwe endelevu kwa manufaa ya taifa.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 25 Januari 2022 na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato alipotembelea bwawa hilo kuona hali halisi ilivyo ambapo kutokana na kujaa maji, aliwahakikishia wananchi kwamba maji yaliyopo yanatosha kuzalisha umeme.

Wakati wa ziara yake ya kukagua bwawa hilo la kuzalisha umeme la Kihansi, alisema ameridhishwa na kiwango cha maji ambacho kimechangiwa pia na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali.

Mradi wa Kihansi una uwezo wa kuzalisha umeme megawati 180 kutoka kwenye mitambo mitatu ambapo kila mtambo unazalisha megawati 60.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akikagua kina cha maji katika bwawa la kufua umeme la Kihansi mkoani Iringa wakati alipofanya ziara mkoani humo. Wengine katika picha ni Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).*

"Mwisho wa mwaka jana (2021) Taifa lilipata shida ya umeme kwa sababu maji yalipungua kwenye mabwawa yanayopeleka maji kwenye mitambo ya kuzalisha umeme ya Ruvu, Kidatu na Kihansi na tukumbuke Waziri wa Nishati, January Makamba alifika kuona hali halisi," alisema Byabato.

Alisema amefanya ziara hiyo baada ya kutumwa na Waziri wa Nishati ili kuona mambo yalivyo kwenye mabwawa ya kufua umeme.

Maji katika bwawa la Kihansi yamefikia ujazo wa mita 1,145 kati ya mita 1,147 kutoka usawa wa bahari, hivyo kiwango cha maji yaliyopo kinatosha kuzalisha umeme.

Alisema wataalam wamemuhakikishia kwamba endapo mvua zitaendelea kunyesha hadi mwezi wa pili mwaka huu katika mikoa ya Iringa na Morogoro, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) litakuwa na uwezo wa kusambaza umeme kwa uhakika.

Aidha akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua mradi

# Jamii yatakiwa kutunza mazingira kuzunguka mabwawa ya umeme

huo, Byabato alitaja bwawa la Kidatu kama mradi mkubwa kwani linazalisha umeme megawati 200 ambazo huunganishwa katika gridi ya taifa.

Baadhi ya changamoto zilizobainika wakati wa ziara hiyo ni pamoja na watu kufanya shughuli za kilimo jiranii na vhanzo vya maji, jambo ambalo linatishia uharibifu wa mazingira na hivyo maji kupungua kiasi cha kuathiri uzalishaji wa umeme nchini.

Umeme unaozalishwa katika bwawa la Kihansi lililopo Iringa na mitambo yake ya kufua umeme ikiwa mkoani Morogoro unaunganishwa kwenye gridi ya Taifa na unatumika katika mikoa yote inayotumia umeme wa gridi ya taifa.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ( wa Pili kushoto) akiwa katika bwawa la kufua umeme la Kihansi mkoani Iringa wakati alipofanya ziara mkoani humo. Wengine katika picha ni Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa kwanza kulia) akiangalia mitambo ya kufua umeme katika bwawa la kufua umeme la Kihansi mkoani Iringa wakati alipofanya ziara mkoani humo. Wengine katika picha ni Wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).*

Katika ziara hiyo, Byabato alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Wizara ya Nishati ili itekeleze majukumu yake ya kila siku kwa ufanisi mkubwa.

## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI KUHUSU UPATIKANAJI WA MSHAURI ELEKEZI (TRANSACTION ADVISOR) WA SERIKALI KATIKA MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA *(LIQUEFIED NATURAL GAS [LNG] PROJECT)*

***25 Januari, 2022***

Mnamo tarehe 25 Januari 2022, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya Baker Botts (UK) LLP walisaini Mkataba wa Huduma ya Ushauri wa Kitaalam na Kampuni ya Baker Botts (UK) LLP ya Uingereza ili kushirikiana na Serikali katika majadiliano ya kutekeleza Mradi wa LNG.

Mchakato wa kumpata Mshauri Elekezi ulianza tarehe 12 Aprili 2018 ambapo TPDC ilitoa tangazo katika magazeti na tovuti mbalimbali kwa ajili ya kualika kampuni mbalimbali kuonesha nia ya kutekeza jukumu hilo kwa Serikali. Tangazo hili lilichapishwa katika gazeti la Dailynews la tarehe 12 Aprili 2018 pamoja na kuwekwa katika tovuti za TPDC, UNDP na AfDB. Hadi kufikia tarehe 4 Mei 2018, kampuni 64 ziliwasilisha nia ya kushiriki katika zabuni tajwa.

Tathmini ya maombi yote ilifanyika kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Mwaka ya 2011 ambapo Kampuni 3 kati ya 64 zilifanikiwa kutimiza vigezo vyote vilivyotumika katika tathmini na hivyo kuendelea na hatua

zinazofuata ambayo ilihusisha ufunguzi wa mapendekezo ya kifedha (*Financial Proposal*). Hata hivyo, mchakato wa zabuni ulisimama kutokana na kusimamishwa kwa majadiliano baina ya Serikali na Wawekezaji.

Mwezi Novemba 2021, Serikali na Wawekezaji walikubaliana kuendeleza majadiliano. Hivyo, TPDC ilihuisha mchakato wa kumpata Mshauri Elekezi baada ya kushauriana na taasisi mbalimbali zinazosimamia manunuzi ya umma na mikataba. Mchakato huu ulikamika na kupelekea TPDC na Mzabuni aliyeshinda kusaini Mkataba tarehe 25 Januari, 2022.

Ikumbukwe kuwa Mradi wa LNG, ni mradi mkubwa na wa kwanza kutelekezwa hapa nchini. Mradi huu unahusisha kuvuna gesi asilia kutoka kwenye kina kirefu cha Bahari takribani kilometa tano kutoka usawa wa Bahari na kuisafirisha takribani kilometa 200 mpaka ufukwe wa Bahari ya Hindi katika eneo la Likong'o, Lindi kwa ajili ya kuichakata na kuisindika ili kuisafirisha kwenye masoko ya kimataifa na gesi nyingine kutumika kwa mahitaji ya ndani na ya kikanda. Mradi huu unatarajiwa kuwa na gharama ya takribani Shilingi trilioni sabini (70).

Kutokana na ukubwa na upekee wa Mradi huu, Serikali iliona umuhimu wa kushirikana na Mshauri Elekezi mwenye uzoefu wa utekelezaji wa miradi ya aina hii duniani ili kushauri kuhusu masuala ya kiufundi, kiuchumi, kifedha na kisheria. Serikali ina lengo la kumtumia Mshauri Elekezi kwa ajili ya kupata ushauri stahiki hususani katika masuala ya teknolojia, kifedha na masoko ya kimataifa ili kuuza gesi iliyogundulika katika misingi ya ushindani na kulinda maslahi ya Taifa.

Kampuni ya Baker Botts (UK) LLP ni moja ya kampuni kubwa Duniani yenye uzoefu wa kimataifa wa kutoa ushauri wa kitaalam kwenye miradi ya aina hii. Kampuni hii itashirikiana na kampuni nyingine za kimataifa zenye ubobezi wa masuala ya teknolojia, kifedha na masoko. Vilevile, Kampuni hiyo itafanya kazi na Kampuni ya Kitanzania ya Apex Attorneys Advocates. Pia Kampuni hiyo itatoa mafunzo maalum kwa watanzania katika mada mbalimbali kuhusu Mradi ili kuwajengea uwezo wakati wa utekelezaji wa Mradi.

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano

**SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA**

**JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**




*www.nishati.go.tz*

*Wizara ya Nishati*

*@Nishati2017*

*wizara_ya_nishati_tanzania*

*Wizara ya Nishati*

***Fika Ofisi ya Mawasiliano,***
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148